Bajeti ya Wananchi



Tafsiri rahisi ya Bajeti ya Taifa 2010/11.

policy forum

Plot 270 KIKO AVENUE Mikocheni B
S.L.P. 38486 Dar es Salaam Tanzania
Simu: +255 22 2772611/+255 782 317434
Nukushi: +255 22 2701433
Barua pepe: info@policyforum.or.tz
Tovuti: www.policyforum.or.tz

policy forum

Shukurani

Chapisho hili limeandaliwa na kikundi kazi cha bajeti cha Policy Forum. Kiolezo kilikubaliwa na kikundi kazi kupitia msaada wa International Partnership. Taarifa za sekta husika ziliandaliwa na HakiElimu (Elimu), World Vision (Kodi na Mapato), SIKIKA (Afya), Policy Forum (Kilimo na Maji), vilevile ndiyo iliyoratibu uhariri wa chapisho hili. Katuni zimechorwa na Nathan Mpangala. Shukurani za pekee ziwaendee SIKIKA kwa kuhakiki umakini chapisho hili pamoja na Agenda Participation 2000 kwa usimamizi makini.

© Policy Forum 2010

Policy Forum,
P. O. Box 38486 Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2772611
Simu: 0782 317431 Fax: +255 22 2701433
www.policyforum.or.tz ® info@policyforum.or.tz

ISBN: 978-9987-9157-9-8

Nakala la jarida hili linaweza kuchapishwa kwa matumizi ya kielimu au yasiyo ya kibiashara kwa kutambua au kukiri chanzo na kutuma nakala Policy Forum.

Bajeti ya Wananchi

Tafsiri rahisi ya Bajeti ya Taifa 2010/11.

1. Bajeti ya Wananchi ni Nini?

Bajeti ya wananchi ni muhtasari uliofupishwa na kurahisishwa kutoka kwenye bajeti ya serikali katika mfumo ambao unawafanya wananchi kuweza kuelewa kirahisi masuala ya msingi yaliyopangwa na serikali katika mwaka husika wa fedha. Bajeti ya wananchi inataja kwa ufupi kabisa wapi serikali itakusanya fedha na namna ilivyopanga jinsi ya kutumia.

Kwanini ni muhimu kwa Tanzania?

Kwa miaka mingi sasa, Tanzania haijawahi kuwa na nyaraka zinazopatikana kirahisi zinazotoa muhtasari wa bajeti ya serikali kwa namna ambayo inaeleweka na kuendana na wananchi wa kawaida. Bajeti hii ya wananchi ni ya kwanza katika kujaribu kufanya taarifa za mambo ya bajeti nchini Tanzania ziweze kupatikana kirahisi na kuwavutia watu wa kawaida ikiwa pamoja na kuwapa fursa ya kujihusisha zaidi katika mchakato wa mipango na matumizi ya serikali.

Nchi zingine kama vile Uganda, Afrika Kusini na India zimekuwa zikitoa bajeti ya wananchi kwa muda mrefu sasa katika jitihada za kufanya taarifa za bajeti zipatikane kwa wananchi na kuwahamasisha wazidi kushiriki katika namna serikali inavyotumia fedha zao.

2. Nyaraka za Bajeti kwa Tanzania

Ifuatayo ni orodha ya nyaraka zinazochapishwa na Serikali na kutumika kama vyanzo vya taarifa za kuandaa bajeti:

- Muundo wa Sera ya Uchumi Mpana: hutoa taarifa za sera ya kodi na marekebisho yake,
- Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, ambayo ifikapo 2025 Watanzania watakuwa wameelimika vizuri na kuwa na uwezo wa kujikimu kiuchumi; pia serikali itakuwa na uwezo wa kuwatumikia watu na uchumi utakuwa imara na wa ushindani,
- Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini, awamu ya pili (MKUKUTA II), kutoka mwaka 2010 hadi 2015. Unalenga katika kutumia ukuaji wa uchumi kushughulikia umaskini, na kwa upekee unasisitizia mchango wa kilimo katika suala hili,
- Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDGs) ambayo yanalenga katika kutokomeza umaskini uliokithiri pamoja na njaa, kutoa elimu kwa wote, kujenga usawa wa kijinsia, kuboresha afya ya mama na mtoto, kupambana na VVU/UKIMWI, kuhifadhi mazingira endelevu na kujenga ushirikiano wa kimataifa,
- Sera na Mikakati ya Kisekta,
- Mikataba ya Ndani na Nje kama vile Mfumo wa Tathmini ya Ufanisi,
- Ilani ya chama tawala,
- Mapendekezo ya "Tume ya Fedha ya Pamoja" (Joint Finance Commission),
- Hotuba ya bajeti za wizara, idara na wakala za serikali,
- Matamko ya aina 3 yanayotokana na Ushauri wa Mapitio ya Matumizi ya Umma kwa Mwaka,
- Mipango ya Muda wa Kati na Taarifa za Muundo wa Matumizi ya Muda wa Kati
- Vitabu Vinne vya Bajeti: cha kwanza ni makisio ya mapato, cha pili na cha tatu ni makisio ya matumizi ya kawaida ya wizara, idara, mikoa na mamlaka za serikali za mitaa; na cha nne ni muswada wa sheria ya fedha ya mwaka husika,
- Muswada wa Matumizi ya Fedha,
- Muswada wa Sheria ya Fedha,
- Hotuba ya Hali ya Uchumi,
- Utafiti wa Bajeti ya Serikali, na
- Makadirio ya Mapato na Matumizi.

3. **Je, serikali inataka kufanikisha nini katika mwaka wa fedha wa 2010/11?**

Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2010/11, kama ilivyoainishwa hapo juu, imezingatia Malengo ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Malengo ya Maendeleo ya Milenia na awamu ya pili ya Mkakati wa Taifa wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini kwa kifupi MKUKUTA II.

Kwa ujumla, bajeti ya mwaka huu inazingatia athari ya mdororo wa kiuchumi duniani na tayari hili limebainishwa kwenye vyombo vya habari kama bajeti ya 'kunusuru' au 'kuchochea' uchumi. Hii inamaanisha kuwa inajaribu kuwapunguzia makali wenye kipato kidogo, kuinua sekta muhimu kama kilimo, kuendeleza ardhi, nishati na miundombinu, na kubuni ajira kwa kupunguza gharama za uzalishaji viwandani kupitia unafuu wa kodi.

Vipaumbele vya Bajeti ya 2010/2011:

	Sekta	2009/10 bajeti (Ktk bilioni)	2010/11 bajeti (Ktk bilioni)	Ongezeko la asilimia
A	Elimu	1,743.9	2,045.3	17.2
B	Miundombinu	1,096.6	1,505.1	37.3
C	Afya	963.0	1,205.9	25.2
D	Kilimo	666.9	903.8	35.5
E	Maji	347.3	397.6	14.5
F	Nishati	285.5	327.2	14.6

***Kumbuka**: Baada ya sekta zilizotajwa hapo juu kutengewa fedha, kinacho fuata ni kujua ni kiasi gani kila wizara itatengewa kutoka kwenye mgao wa sekta. Baadhi ya wizara zinatengewa fedha kutoka sekta mbalimbali wakati wizara nyingine hupata kutoka sekta moja (mfano; bajeti ya sekta inaweza ikajumuisha fedha zitakazotengewa katika wizara pamoja na fedha zitakazotengewa Serikali za Mitaa).*

Muhtasari wa baadhi ya bajeti za wizara kwa sekta zilizotajwa hapo juu unaoneshwa zaidi chini.

4. Je, fedha huwa zinatoka wapi na kiasi gani?

Jumla ya fedha zote zilizopangwa kutumika kwa mwaka 2010/11 ni Shs. bilioni 11, 112.419 au takribani Shs. trilioni 11. Serikali inapanga kukusanya kiasi hiki kutokana na mapato ya ndani (kodi na mapato mengine yasiyotokana na kodi), mikopo ya ndani (fedha zinazotafutwa ndani), na misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo (fedha zinazotafutwa nje).

Muundo wa Bajeti 2010/11

Mapato	Jumla ndogo	Shs. (bilioni)
Mapato ya Ndani		6,003.59
Mapato yanayotokana na Kodi (TRA)	5,652.59	
Mapato yasiyotokana na kodi	351.00	
Vyanzo vya Mamlaka za Serikali ya Mitaa		172.58
Misaada na Mikopo ya Nje - Bajeti ya Msaada wa Jumla		821.65
Misaada na Mikopo ya Nje - Mfuko wa Misaada ya Miradi		2,452.91
Misaada na Mikopo kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo	1,975.12	
Mfuko wa Misaada na Mikopo	477.78	
Mikopo ya Ndani na Nje		1,331.212
Mikopo ya Ndani		797.62
Mapato ya Ubinafsishaji		30.00
Mapato ya Jumla	**8,456.49**	**11,609.56**

i. Fedha za ndani: Shs. bilioni 5,652.59

Asilimia kubwa ya fedha za ndani yaani Shs. bilioni 5,652.59 yatakuwa ni mapato yanayotokana na kodi. Shs. bilioni 351.00 ni mapato yasiyotokana na kodi Shs. bilioni 30 zitatokana na mapato ya ubinafsishaji.

Hii inamaanisha kuwa japo sehemu ya fedha hizi itakusanywa kutoka katika makampuni kupitia malipo ya kodi ya ushirika, kiasi cha kutosha kitatokana na Watanzania wa kawaida wakilipa kodi ya mapato, kodi ya ongezeko la thamani, ushuru, kodi za magari na kodi ya mali zisizohamishika kama nyumba, nakadhalika. Na kwahiyo hii ni **FEDHA YA WANANCHI**.

Ifahamike kuwa hii ni fedha ambayo serikali bado haijakusanya. Uzoefu kutoka miaka iliyopita unaonesha kuwa makusanyo yamekosa mipango; hivyo basi baadhi ya hatua ambazo serikali inakusudia kuchukua ili kukusanya fedha zote ilizopanga kukusanya mwaka huu ni pamoja na:

- Kusajili walipa kodi wapya,
- Kuimarisha mifumo ya ukusanyaji kodi,

- Kuongeza mapato ya utalii kwa kuboresha viwango vya hoteli,
- Kukusanya fedha za ziada zinazotokana na mashirika na taasisi za umma,
- Kuongeza ukusanyaji wa mapato yasiyotokana na kodi, na
- Kujenga uwezo katika ngazi ya Serikali za Mitaa kuimarisha tathmini na ukusanyaji wa mapato.

ii. Fedha za nje (kutoka kwa washirika wa maendeleo): Shs. bilioni 3, 274.553

Fedha zinazotokana na vyanzo vya nje ya Tanzania zinaweza kukusanywa ama katika utaratibu wa bajeti ya misaada ya jumla au mikopo na ruzuku. Bajeti ya misaada ya jumla inahusisha michango ya moja kwa moja inayotolewa na washirika wa maendeleo kwa serikali ya Tanzania, hususan kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Inaweza kusitishwa ikiwa washirika wa maendeleo wataona serikali haikidhi masharti fulani maalum, hasa yanayohusiana na utawala bora. Kwa mwaka huu mchanganuo uko kama ifuatavyo:

- Shs. bilioni 821.645 kama bajeti ya misaada ya jumla, na
- Shs. bilioni 2,452.908 kama misaada na mikopo.

Washirika wa maendeleo wa Tanzania ni Uingereza, Denmark, Uholanzi, Ubelgiji, Canada, China, Ufini (Finland), Ufaransa, Ujerumani, Ireland, Italia, Japan, Korea Kusini, Kuwait, Norway, Hispania, Uswidi (Sweden), Uswisi (Switzerland), Marekani, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Kiuchumi Afrika, Umoja wa Ulaya, Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Mfuko wa Kuwait, Mfuko wa Nchi za Nordic, Mfuko wa OPEC, Mfuko wa Saudia na Mashirika ya Umoja wa Kimataifa.

iii. Kuazima kutoka kwenye taasisi za fedha: Shs. bilioni 2,128.832

Serikali inapanga kuazima kiasi hiki kutoka katika masoko ya fedha ya ndani na nje kwa ajili ya kufadhili bajeti ya maendeleo (hususan kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya vipaumbele).



5. Matumizi

a. Matumizi ya Kawaida: ni jumla ya kiasi cha fedha ambacho serikali hutumia kuendesha kazi zake. Inajumuisha mishahara ya watumishi wa umma, malipo ya riba kwenye mikopo iliyochukuliwa na serikali, pango na gharama za mafuta.

Kwa mwaka wa fedha wa 2010/11 serikali inapanga kutumia **Shs. bilioni 7,790.506.** Kwa mwaka 2009/10 serikali ilitumia **Shs. bilioni 4,189.721**.

b. Matumizi ya Maendeleo: inamaanisha fedha itakayotumika kwa ajili ya kazi kama vile ujenzi wa shule, hospitali na barabara, ambao utapelekea kuboresha utoaji huduma kwa Mtanzania wa kawaida. Matumizi hayo yanahusiana kwa karibu na mabadiliko yanayoonekana katika ubora wa maisha.

Kwa mwaka wa fedha wa 2010/11 serikali inapanga kutumia **Shs. bilioni 3,819.051** au **asilimia 33** ya jumla ya bajeti yote. **Shs. bilioni 1,954.197** ilitumika mwaka 2009/10.

Ni muhimu sana kwamba fedha ilete maendeleo. Wananchi wanapaswa kuona mabadiliko halisi katika elimu, afya, miundombinu na upatikanaji wa maji safi na salama ifikapo Juni 2011.

6. Je, kitu gani kimebadilika katika bajeti ya 2010/11?

1) **Kodi:** Mwaka 2009/10, mpango ulikuwa kupanua wigo wa kodi, kupunguza misamaha ya kodi, kudhibiti ukwepaji kodi, kuhamasisha ulipaji kodi na kuweka utaratibu wa kutathmini kodi katika biashara. Katika kuelekea kuboresha mfumo wa kodi, msisitizo katika mwaka 2010/11 utakuwa kutafuta vyanzo vipya vya mapato na njia nzuri za ukusanyaji kodi. Mabadiliko mengi yanalenga katika kuinua sekta za kilimo na uzalishaji.

2) **Wafanyakazi:** Kodi ya mapato ilikatwa asilimia moja na mshahara wa kima cha chini kwa sasa umepangwa kuongezwa japo bado haijatangazwa rasmi lini na kiasi gani kitaongezwa.

3) **Wakulima:** Kodi ya ongezeko la Thamani imeondolewa kwenye usafirishaji wa bidhaa za ndani za kilimo nchini, zana za kilimo, uzalishaji maziwa (usafirishaji, ufungashaji na usindikaji) na ufungashaji wa matunda.

4) **Wazee na walemavu:** Kodi imeondolewa kwenye umiliki wa mali zisizohamishika kama nyumba.

5) **Madini:** kuweka wigo wa ukomo wa maeneo ya uchimbaji.

6) **Magari:** Ongezeko la jumla katika ada zote za usajili.

7) **Viwanda:** Ushuru umepunguzwa kwenye mafuta mazito ya kuendeshea mitambo. Kupunguza gharama za uzalishaji viwandani kutapelekea kuongezeka kwa ajira.

8) **Vifaa vya ujenzi:** Kutoa unafuu maalum wa kodi ya ongezeko la thamani kwenye maeneo ya uwekezaji na uzalishaji wa bidhaa za kuuza nje (EPZ/SEZ)

7. Maboresho ya kisera

Kwa mtazamo wa kupanua wigo wa utozaji kodi na kuimarisha ukusanyaji mapato ili kugharamia matumizi, serikali ilipendekeza kufanya marekebisho yafuatayo:

A. Marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani: Kuwezesha Kilimo Kwanza

- Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye usafirishaji wa mazao ya kilimo.
- Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mashine na vifaa vya kukusanya, kusafirisha na kusindika maziwa na mazao ya maziwa.
- Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mashudu kwa ajili ya chakula cha mifugo.
- Kutoa unafuu maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifaa vinavyouzwa kwa wataalamu wa mifugo waliosajiliwa.
- Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye zana za kilimo kama vile mashine za kuvuna nafaka na kukatia majani.
- Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani katika usafirishaji wa maua kwa ndege kwenda nje ya nchi.
- Kutoa unafuu maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mabanda yanayotumika katika kilimo cha maua (green houses).
- Kutoa unafuu maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye uuzaji wa bidhaa na huduma zitolewazo kwa wakulima waliosajiliwa au mashamba ya vyama vya ushirika kwa ajili ya kujenga miundombinu ya mashamba kama vile mitaro ya umwagiliaji, barabara mashambani na ujenzi wa maghala.
- Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za kuzalisha mifugo kwa njia ya kupandisha kwa kutumia mashine maalum za kuzalishia/kutotolea vifaranga.

B. Kwa mtazamo wa kuhamasisha uwekezaji na kuboresha tija katika sekta ya viwanda, serikali ilipendekeza kufanya marekebisho yafuatayo:

- Kutoa unafuu maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye uuzaji wa vifaa vya ujenzi na huduma za ujenzi kwa waendelezaji wa maeneo ya uwekezaji na uzalishaji wa bidhaa za nje (EPZ/SEZ).
- Kutoa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri kwenye usindikaji na uzalishaji wa mafuta ya kula kwa wazalishaji wanaotumia mbegu za mafuta zinazozalishwa hapa nchini.
- Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vifungashio vya juisi za matunda na bidhaa za maziwa.
- Kurejesha utaratibu wa kutambua au kuweka katika madaraja baadhi ya vifaa vinavyotumika katika vitega uchumi maalum kama bidhaa za mtaji ili kutoa unafuu wa kodi kwa wawekezaji.

Yote haya kwa pamoja yatapunguza mapato ya serikali kwa **Shs. bilioni 2.391**.

C. Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato:

- Kurekebisha kifungu cha 11 cha sheria ya kodi ya mapato ili kuweka wigo wa ukomo wa maeneo ya uchimbaji wa madini katika maeneo ya uchimbaji madini.
- Kupunguza kiwango cha chini cha Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi kutoka asilimia 15 hadi 14 sambamba na nyongeza ya kima cha chini cha mshahara.
- Kuongeza muda wa kodi ya zuio kwa wauzaji wa bidhaa na watoa huduma wote waliosajiliwa na wasiosajiliwa namba zao za utambulisho wa mlipa kodi ili kuwahamasisha wasiokuwa na namba za utambulisho wakasajiliwe.

Yote haya kwa pamoja yatapunguza mapato ya serikali kwa **Shs. bilioni 4.468**.

D. Marekebisho ya Sheria ya Ushuru wa Bidhaa

- Kupunguza ushuru wa bidhaa kwenye mafuta mazito kutoka sh. 97 hadi Shs. 80 kwa lengo la kupunguza gharama za uzalishaji viwandani.
- Kurekebisha kwa asilimia 8 viwango maalum vya ushuru wa bidhaa zinazotozwa kwa bidhaa zisizokuwa za petroli.
- Marekebisho ya viwango vya ushuru wa bidhaa kwenye sigara.

E. Marekebisho kwenye Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa

- Kusamehe kodi ya majengo kwenye nyumba wanazoishi wazee wenye umri wa zaidi ya miaka 60 na walemavu ambao hawana vyanzo vya mapato.
- Kupitia upya kiwango cha kutoza ushuru wa mazao ya kilimo kiwe kati ya asilimia 3 na 5 ya kuuza mazao mashambani.

F. Marekebisho kwenye Kodi ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki wa Magari:

- Ada ya kusajili gari imeongezeka kutoka Shs. 120,000 hadi Shs. 150,000
- Ada ya kusajili pikipiki imeongezeka kutoka Shs. 35,000 hadi Shs. 45, 000

Yote haya kwa pamoja yataongeza mapato ya serikali kwa **Shs. bilioni 3.19.**

G. Marekebisho kwenye Sheria ya Usalama Barabarani:

Ujazo wa injini ya gari	Kodi ya zamani (Kwa mwaka)	Kodi mpya (Kwa mwaka)
0-500. cc	30,000/=	50000/=
501-1500.cc	50,000/=	100,000/=
1501-2500.cc	100,000/=	150,000/=
Zaidi ya 2501.cc	150,000/=	200,000/=

Yote haya kwa pamoja yataongeza mapato ya serikali kwa **Shs. bilioni 16.981**

H. Marekebisho kwenye Sheria ya Bodi ya Korosho

- Kuongeza kiwango cha ushuru wa kusafirisha nje korosho ghafi kutoka asilimia 10 hadi 15 ya thamani au Dola .za Marekani 160 kwa tani moja kwa kutegemea ni kiwango kipi kikubwa.

Hii itaongeza mapato ya serikali kwa **Shs. bilioni 2.613**

I. Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Michezo ya Kubahatisha

- Kuongeza kiwango cha kodi inayotozwa kwenye mashine za michezo ya kubahatisha kutoka Shs. 16,000 hadi Shs. 32,000 na kutoza kodi ya kiwango cha asilimia 13 ya mapato ya Tombola.

Hii itaongeza mapato ya serikali kwa **Shs. bilioni 0.5**

8. Mipango thabiti ya matumizi yaletayo matokeo

Malekezo kwa ufupi kuhusu mipango ya matumizi kwa ajili ya sekta za elimu, afya, maji safi na salama na kilimo, ni kama yafuatayo:

Elimu

Je, nini lengo kuu la jumla la serikali kwa sekta hii katika mwaka ujao wa fedha?

Jumla ya bajeti iliyopangwa kwa sekta ya elimu kwa mwaka 2010/2011 ni Shs. trilioni 2.0453, ambalo ni ongezeko la asilimia 17.2 ikilinganishwa na trilioni Shs. 1.744 za mwaka jana.

Jedwali hapo chini linabainisha kiasi gani cha pesa hizo kitatumika na **Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (WEMU)** katika matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo, na kulinganisha na mwaka 2009/2010.

Mchanganuo	2009/2010	2010/2011
Matumizi ya Kawaida	428,436,913,000	525,940,530,000
Matumizi ya Maendeleo	129,283,697,000	139,632,007,000
Jumla ya Bajeti	557,720,610,000	665,572,537,000

Kwa mwaka 2010/2011, **bajeti ya WEMU** ni asilimia 32.5 ya bajeti ya jumla ya sekta ya elimu. Wakati huo huo, asilimia 67.5 ya fedha zilizotengwa kwa ajili ya elimu itatumiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa, zinazofanya kazi karibu na wananchi.
Taarifa zingine zilizotolewa zinahusiana na bajeti ya WEMU.

Je, fedha zinatoka wapi?

Sehemu kubwa ya fedha ambazo WEMU inapanga kutumia kwa mwaka huu - takribani **Shs. bilioni 582.15**, itatokana na vyanzo vya ndani. Idara zitachangia **Shs. bilioni 83.42** kwenye bajeti ya WEMU kwa mwaka 2010/2011.

Je, vidokezo vya bajeti ni vipi?

Vipaumbele vya kisera vya serikali katika elimu ya msingi na sekondari kwa mwaka huu wa fedha vinazingitia awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM II) na awamu ya pili ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MMES) uliozinduliwa hivi karibuni. Baadhi ya vidokezo vya mwaka huu ni:

Elimu ya Msingi

- Kupitia upya MMEM II kwa kusudi la kuelekeza mchakato wa kuandaa MMEM III,
- Kutoa mafunzo kwa makatibu wa elimu katika ngazi ya kata, wilaya na mkoa,
- Kuajiri walimu 14,501 wa shule za msingi katika shule za msingi za serikali,

- Kuhamasisha jamii kuwaandikisha watoto kwa ajili ya elimu ya awali,
- Kukarabati baadhi ya shule za msingi,
- Kuwaandikisha watoto wapatao 2,043,984 katika ngazi hii,
- Kusimamia matumizi ya rasilimali chini ya MMEM II, na
- Kujenga uwezo kwa walimu na makatibu wapatao 200.

Elimu ya Sekondari

- MMES II utaanza kutekelezwa. Una jumla ya bajeti ya Dola za Marekani milioni 470 kwa miaka mitano na lengo lake ni kuboresha kiwango cha kufaulu katika hisabati, sayansi na kiingereza,
- Utekelezaji wa mwaka huu wa MMES II umetengewa Shs. bilioni 150. Malengo makuu ya mwaka huu ni pamoja na kutoa ruzuku ya mtaji kwa shule za sekondari kwa ajili ya kufundishia na kununulia vifaa vya kujifunzia, kujenga maabara na nyumba za walimu, na kuboresha ufanisi wa wanafunzi katika kufaulu hisabati, sayansi na kiingereza. na
- Kuajiri walimu wapatao 17,204 katika shule za sekondari za serikali ili kuweza kuongeza idadi ya wastani ya walimu hadi kufikia watano katika kila shule.

Mafunzo ya Ufundi

- Kuendelea na mipango ya utekelezaji wa kujenga vyuo 28 vya ufundi VETA katika ngazi ya wilaya na kumalizia ujenzi wa vyuo vya ufundi katika mikoa ya Pwani, Manyara, Lindi na Dar es Salaam, na
- Kulipia mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi 700 katika chuo cha ufundi Arusha.

Elimu ya Juu

- Kulipia masomo wanataaluma 80 katika elimu ya juu ya vyuo vya umma,
- Kuajiri wahadhiri na wafanyakazi katika elimu ya juu ya vyuo vya umma,
- Kujenga ofisi na kukarabati miundombinu katika vyuo vikuu vya umma,
- Kuongeza udahili wa wanafunzi hadi kufikia 89,617 katika taasisi za elimu ya juu wanaoweza kupata mikopo. Shs. bilioni 240 zimetengwa kwa ajili ya mikopo hiyo, na
- Kulipia wanafunzi 1,750 kuchukua shahada ya kwanza ya madawa.

Afya

Je, nini lengo la jumla la serikali kwa sekta hii katika mwaka ujao wa fedha?

Bajeti ya jumla iliyotengwa kwa ajili ya sekta ya afya kwa mwaka 2010/11 ni Shs. trilioni 1.205 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 25.2 ikilinganishwa na Shs. bilioni 963 zilizotengwa mwaka 2009/2010.

Jedwali hapo chini linabainisha kiasi gani cha fedha kitatumiwa na **Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii (WAUJ)** katika matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

Mchanganuo	2009/10	2010/2011
Matumizi ya Kawaida	244,895,993,044	229,978,968,000
Matumizi ya Maendeleo	260,599,867,000	448,442,515,000
Bajeti ya Jumla	505,495,860,044	678,421,483,000

Kwa mwaka 2010/2011, **bajeti ya WAUJ** ni asilimia 56.2 ya bajeti yote ya sekta ya afya.

Maelezo yanayofuata hapa chini yanahusu bajeti ya WAUJ:

Je, fedha zinatoka wapi?

WAUJ imekadiria kukusanya jumla ya Shs. bilioni 2.486 kutoka katika vyanzo vya ndani. Mchanganuo wa bajeti ya matumizi ya kawaida ni kwamba Shs. bilioni 105 zitatumika katika gharama zingine wakati Shs. bilioni 124 zitatumika kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi wa wizara na taasisi zilizo chini yake. Kwa kiasi cha fedha zitakazotumika kwa ajili ya matumizi ya maendeleo, Shs. bilioni 9.873 zitatolewa na serikali wakati Shs. bilioni 438.5 zitatolewa na washirika wa maendeleo.

Je, vidokezo vya bajeti ni vipi?

Vipaumbele vya serikali kwa kuzingatia masuala ya msingi katika sekta ya afya vimewekwa kama ifuatavyo:

Malaria

- Huduma za kinga ikiwa pamoja na kugawa vyandarua katika kila kaya,
- Kukarabati maabara katika hospitali 10 za wilaya, kununua na kugawa madawa na vifaa vya matibabu katika hospitali za umma.

Afya ya mama na mtoto

- Kununua na kugawa madawa, vifaa vya kujifungulia na kupanga uzazi.

VVU/UKIMWI

- Kuongeza vituo vya kutolea huduma ya VVU/UKIMWI kutoka 909 hadi 1400, na kuongeza huduma ya matibabu kwa watu wanaoishi na VVU/UKIMWI kutoka 337,854 hadi 440,000,
- Kuongeza vituo vya huduma ya kinga ya maambukizi VVU/UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto kuanzia 3,626 hadi 4,200, na vituo vya maambukizi ya awali ya VVU kwa watoto wachanga na wanawake walioambukizwa VVU kutoka vituo 730 hadi 1,200.

Ustawi wa jamii

- Huduma za jamii ikiwa pamoja na kutafsiri sheria katika Kiswahili kwa watu wenye ulemavu, Sheria ya Moto, Sheria ya Mtoto, na Sheria ya Biashara Haramu ya Kusafirisha Watu,
- Kukarabati vyuo vikuu vitatu vinavyofundisha ustawi wa jamii,
- Kujenga mahakama ya watoto Mtwara na kituo cha wazee Morogoro,
- Kuendelea kujenga ofisi ya idara ya ustawi wa jamii Dar es Salaam.

Rasilimali watu na mafunzo

- Kujenga uwezo kwa watumishi wa umma katika sekta za afya na huduma kwa jamii ili kuboresha utoaji huduma,
- Kuboresha taasisi ya mafunzo nje ya darasa au kwa njia ya posta Morogoro.

Mengineyo

- Ukaguzi katika migodi na maeneo yanayozunguka migodi, viwanda na vituo vya huduma katika mipaka ya nchi, bandari na viwanja vya ndege,
- Kuanzisha kitengo cha maabara ya upasuaji katika hospitali ya taifa Muhimbili,
- Kununua vifaa vya upasuaji wa moyo kwa ajili ya hospitali ya Bugando,
- Kujenga nyumba ya Waziri wa Afya, na
- Kukarabati nyumba ya Katibu Mkuu wa Wizara na Makao Makuu ya Wizara Dodoma na Dar es Salaam.

Maji na Umwagiliaji

Je, nini lengo kuu la jumla la serikali kwa sekta hii katika mwaka ujao wa fedha?

Bajeti ya jumla iliyopangwa kwa ajili ya sekta ya maji kwa mwaka 2010/11 ni Shs. bilioni 397.6 ambayo ni ongezeko la asilimia 14.5 kutoka Shs. bilioni 347.3 zilizotengwa mwaka 2009/10.

Jedwali hapo chini linabainisha kiasi gani cha fedha kitatumika na Wizara ya Maji na Umwagiliaji (WMU) katika matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

Mchanganuo	2009/2010	2010/2011
Matumizi ya Kawaida	19,277,172,000	18,442,785,000
Matumizi ya Maendeleo	245,656,445	233,092,607,000
Bajeti ya Jumla	264,933,617,000	251,535,392,000

Kwa mwaka 2010/2011, bajeti ya WMU ni asilimia 63.2 ya bajeti yote ya sekta ya maji.

Maelezo yanayofuata hapa chini yanahusu bajeti ya WMU:

Je, fedha zinatoka wapi?

Mchanganuo wa matumizi ya kawaida ni kwamba Shs. bilioni 6.5 itatumika kwa gharama zingine wakati ambapo Shs. bilioni 11.8 zitatumika kwa ajili ya mishahara ya wafanyakazi wa wizara na taasisi zilizo chini yake. Kwa kiasi ambacho kitatumika kwa ajili matumizi ya maendeleo, Shs. bilioni 41.5 zitatokana na serikali wakati ambapo Shs. bilioni 191.5 zitachangiwa na washirika wa maendeleo.

Je, vidokezo vya bajeti ni vipi?

Lengo la serikali kwa mwaka 2010/11 linabaki kuhakikisha kuwa rasilimali ya maji, inaendelezwa na kutumiwa vizuri kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya pamoja ya sekta mbalimbali kwa kuwa na utaratibu thabiti wa kusimamia rasilimali ya maji, kuendeleza na kuboresha miundombinu ya kusambazia maji, huduma za maji taka pamoja na huduma za umwagiliaji.

Vidokezo vya bajeti ya sekta ya maji kulingana na WMU kwa mwaka 2010/11 ni:

- Kuboresha usimamizi wa rasilimali ya maji ikiwa pamoja na kufuatilia mwenendo wa rasilimali ya maji kwa kujenga vituo vya kusimamia maji sambamba na kuweka vifaa vya kupima ujazo na ubora wa maji,
- Kutafuta na kuhifadhi vyanzo vipya vya maji, uchimbaji visima vya maji na kuunda mikakati ya pamoja ya kusimamia na kuendeleza vyanzo hivyo,
- Kuelimisha wananchi kuhusu matumizi endelevu ya rasilimali ya maji sambamba na kuona umuhimu wa kuwa na vibali vya kutumia maji,
- Kuboresha ofisi ya mabonde ya maji ikiwa pamoja na kutambua na kuhifadhi maeneo ya rasilimali ya maji na kuelimisha jamii katika kuanzisha kamati ndogo za mabonde ya maji,
- Kuelimisha wananchi juu ya matumizi sahihi ya ardhi na kuhifadhi mazingira kwa lengo la kuhifadhi na kulinda vyanzo vya maji,
- Kuboresha usimamizi shirikishi wa rasilimali za maji kama mto Nile, ziwa Victoria, mto Zambezi, mto Songwe na mto Ruvuma,
- Kuboresha programu za mazingira na maji safi ikiwa pamoja na miradi kwenye maeneo ya vijijini,
- Kutekeleza miradi ya maji ya kujenga na kupanua usambazaji wa maji safi na mifumo ya maji taka katika maeneo ya vijijini na mijini,
- Kuboresha taasisi za matumizi ya maji na kuboresha ukusanyaji wa ankara za maji,
- Kuendelea kujenga mifumo ya umwagiliaji na matumizi ya teknolojia ya umwagiliaji wenye tija katika kuwezesha kilimo ambacho kinategemea umwagiliaji tu,
- Kutafsiri kwa Kiswahili na kusambaza Sera ya Umwagiliaji na kuendesha kampeni za kuelimisha kuhusu sera ya maji, sera ya umwagiliaji na mikakati ya sekta ya maji,
- Chini ya Taasisi ya Usimamizi na Uendelezaji Maji, kutoa mafunzo kwa mafundi katika sekta ya maji,
- Kuendesha uwezeshaji kwa wakulima na wataalamu wa kilimo kuhusu umwagiliaji,
- Kuendelea na mapambano dhidi ya rushwa na UKIMWI na kujenga uwezo kwa watumishi wa umma kwa kusudi la utoaji bora wa huduma.

Kilimo

Je, nini lengo kuu la jumla la serikali kwa sekta hii katika mwaka ujao wa fedha?

Bajeti ya jumla iliyotengwa kwa ajili ya sekta ya kilimo kwa mwaka 2010/11 ni Shs. bilioni 903.8 ambayo ni asilimia 35.5 ikiwa ni ongezeko kutoka bilioni 666.9 zilizokuwa zimetengwa mwaka 2009/10.

Jedwali hapo chini linabainisha kiasi gani cha fedha kitatumiwa na **Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika (WKCU)** katika matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

Mchanganuo	2009/10	2010/2011
Jumla ya Bajeti	228,564,587,000	253,355,014,000
Matumizi ya Kawaida	135,870,333,044	149,402,643,000
Matumizi ya Maendeleo	92,694,254,000	103,952,371,000

Kwa mwaka 2010/2011, bajeti ya WKCU ni asilimia 28 ya jumla ya bajeti yote ya sekta ya kilimo.

Maelezo yanayofuata hapa chini yanahusu bajeti ya WKCU:

Je, fedha zinatoka wapi?

Mchanganuo wa bajeti ya maendeleo ni kwamba Shs. bilioni 3.4 zitatolewa na serikali wakati ambapo Shs. bilioni 100.5 zitatokana na washirika wa maendeleo.

Vidokezo vya bajeti ya sekta ya kilimo kulingana na WKCU.

Wizara itaendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Kilimo (ASDP) inayolenga katika kuboresha usalama wa chakula na kupunguza umaskini. Inapotekeleza ASDP, wizara itazingatia shabaha muhimu za Malengo ya Maendeleo ya Milenia, MKUKUTA II na KILIMO KWANZA, ambavyo vyote vinalenga katika maendeleo ya kiuchumi, kupunguza umaskini ulikithiri pamoja na njaa. Bajeti ya mwaka 2010/11 imetoa kipaumbele kilimo na maendeleo ya mifugo kama sehemu ya kulenga 'Kilimo Kwanza' ili kuifanya sekta ivutie uwekezaji na kusaidia sekta zingine kwa ajili ya kuongeza tija katika uchumi. Kwa kuongezea katika vipaumbele 2010/11 vilivyoorodheshwa sehemu ya 3 hapo juu, vidokezo katika sekta hii kwa mwaka huu ni:

- Katika moyo uleule wa kuwezesha "Kilimo Kwanza", Kodi ya Ongezeko la Thamani imeondolewa katika usafirishaji wa bidhaa za ndani za kilimo mashambani kama miwa, katani na chai kutoka mashambani kwenda kusindikwa kiwandani. Hata hivyo, hii itatumika kwenye mashamba ya kisasa tu
- Kodi ya Ongezeko la Thamani pia imeondolewa kwenye mashudu ya chakula cha mifugo, zana za kilimo, mashine za kuvuna nafaka, na zile ambazo zinatumika katika kuzalishia na kutotolea vifaranga,
- Kilimo cha maua pia kitafaidika na kusamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ushuru unaotozwa kwa kusafirisha nje ya nchi na kutoa unafuu maalum wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mabanda yanayotumika katika kilimo cha maua,
- Kuongeza ushuru wa forodha kwenye korosho ghafi kutoka asilimia 10 hadi 15 au Dola za Marekani 160 kwa tani moja, kwa kutegemea kiwango kipi ni kikubwa. Hii inakusudiwa kuhamasisha shughuli za kuongeza thamani nchini na kufufua viwanda vya usindikaji korosho, jambo ambalo litasaidia kupatikana kwa ajira.
- Kuendelea na ombi la kiwango cha kodi cha asilimia 10 kwenye ngano kwa mwaka mmoja badala ya kiwango cha asilimia 35,
- Kuondoa ushuru wa kuingiza matrekta na kwa ajili ya ufugaji kuku,

Vingine ni:

- Kutekeleza programu ya ASDP ambayo pia inatekeleza sera ya kupeleka madaraka kwa wananchi (*Decentralization by Devolution – D-by-D*) kwa kupeleka karibu asilimia 75 ya raslimali za Sekta ya Kilimo wilayani na vijijini.
- Utekelezaji wa uwezeshaji wa programu ya sekta ya kilimo wilayani kwa ajili ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa katika wilaya 28, kuanzisha miradi ya umwagiliaji, miradi ya kuyafikia masoko, kuimarisha uwezo na elimu ya kusimamia miradi kwa njia bora katika sekta ya kilimo.
- Kuendeleza utafiti wa urutubishaji udongo kwa njia ya kuendeleza namna mbadala ya usimamizi wa uchanganyaji udongo wenye rutuba na kuhamasisha utumiaji wa mboji.
- Kuongeza usambazaji wa mbegu bora za kahawa na chai.
- Jumla ya Shs. bilioni 3.8 zimetengwa kwa ajili ya mfuko wa zana za kilimo utakaotumika kama mikopo nafuu kwa wakulima wadogo.
- Kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya kilimo kwa kushirikiana na kituo cha uwekezaji. Aidha, kwa kushirikiana na Benki Kuu, kuanzisha benki ya kusaidia kilimo.

- Kuandaa na kupitia upya sheria na kanuni zitumikazo katika sekta ya kilimo ili kuhakikishia zinakidhi matakwa na malengo ambayo sera na sheria zinatungwa kwazo.
- Kuanzisha Tume ya Ushirika ambapo wizara inaomba Shs. bilioni 6.5 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na bilioni 100 kwa ajili ya kazi za maendeleo.
- Kwa ujumla, sera ya KILIMO KWANZA imeamsha ongezeko la kiasi kilichotengwa kwa ajili sekta hii. Mpango wa 'Kilimo Kwanza' kwa sasa ni chombo kinachotumika na serikali kuifanya nchi ipate mapinduzi ya kilimo na kuifanya sekta hii iwe ya kisasa zaidi.

9. Je, utafanya nini na maelezo haya?

Bajeti ya serikali ni kipimo kizuri katika kile serikali **inachopanga kufanya** katika mwaka husika. Kama unataka kujua wapi fedha yako ya kodi inakwenda, iwe kuna mipango ya kuboresha elimu au afya katika eneo lako, basi unaweza kuangalia ni jinsi gani na kiasi gani cha fedha kimetengwa, hususan katika **maendeleo**. Kijitabu hiki kinajaribu katika muhtasari baadhi ya maelezo haya kwa urahisi kadri inavyowezekana. Hata hivyo, unaweza kupata taarifa zaidi za mchakato wa bajeti kutoka:

- Nyaraka za bajeti za Tanzania (angalia kifungu cha 2 kupata orodha ya nyaraka hizi), na hasa **vitabu vinne vya bajeti ya serikali.**
- Wizara ya Fedha na Uchumi, S.L.P 9111, Dar es Salaam, Tovuti:http://www.mof.go.tz
- Ofisi za serikali za mitaa na/au maafisa katika eneo lako kama Afisa Mtendaji Kijiji.
- Policy Forum, S.L.P 38486, Dar es Salaam, website: http://www.policyforum.or.tz Simu: (022) 2772611 / fax: (022) 2701433).

Kumbuka, **ni haki yako kujua** jinsi gani serikali inapanga kutumia **fedha zako**. Zungumza na viongozi wako kuhusu taarifa hii na washirikishe watu wengine katika jamii yako.

Nini mawazo, maswali na maoni yako kuhusu bajeti hii?

Je, unataka taarifa zaidi ya hizi zilizotolewa kwenye kijitabu hiki? Unahitaji taarifa ya aina gani?

Je, una kitu chochote cha ziada unachotaka tujue?

Je, kijitabu kimesaidia? ☐ Ndiyo ☐ Hapana ☐ Kiasi

Je, kijitabu kilikuwa rahisi kusoma na kuelewa? ☐ Ndiyo ☐ Hapana ☐ Kiasi

Tutumie kupitia anuani yetu hapo juu